# PBPA Bulletin

TOLEO Na. 02 | JUNI, 2025




## MIAKA 4 YA RAIS SAMIA: PBPA YANG'ARA KATIKA USIMAMIZI WA MFUMO WA UAGIZAJI WA MAFUTA NCHINI


PbpaTanzania PbpaTanzania pbpa_tanzania



# KAMATI YA UHARIRI

1. **Lilian Rwegumbira**
   Mwenyekiti
2. **Sarah Mwakyusa**
   Katibu
3. **Matiko Sanawa**
   Mjumbe
4. **Henry Kilenga**
   Mjumbe
5. **Rehema Mahundi**
   Mjumbe
6. **Nyamhoni Chacha**
   Msanifu

## Contact Us

The United Republic of Tanzania
Petroleum Bulk Procurement Agency,
P. O. Box 2634,
Dar es Salaam, Tanzania,
info@pbpa.go.tz.
+255 222 129 009

# YALIYOMO


04. MIAKA 4 YA RAIS SAMIA: PBPA YANG'ARA KATIKA USIMAMIZI WA MFUMO WA UAGIZAJI WA MAFUTA NCHINI

08. MFUMO WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA WAENDELEA KUIMARIKA- DKT. BITEKO

10. USHINDANI WAONGEZEKA SEKTA YA MAFUTA – DKT. BITEKO

12. WAZIRI SIMBACHAWENE AWAPONGEZA PBPA

14. PBPA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA KWA MWAKA 2025

16. PBPA YAPUNGUZA UPOTEVU WA MAFUTA KWA TEKNOLOJIA YA SCADA

18. PBPA YAFANYA MAFUNZO YA ULINZI WA MTOA TAARIFA

20. MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF) UMETOA ELIMU KWA WATUMISHI WA OFISI YA WAKALA WA UAGIZAJI MAFUTA KWA PAMOJA (PBPA)




# MIAKA 4 YA RAIS SAMIA: PBPA YANG'ARA KATIKA USIMAMIZI WA MFUMO WA UAGIZAJI WA MAFUTA NCHINI

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Nishati imeendelea kushuhudia mageuzi na mafanikio makubwa, hususan katika uratibu wa uagizaji wa bidhaa za mafuta nchini. Kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Serikali imefanikiwa kuboresha upatikanaji, usimamizi na ufanisi wa mnyororo wa uagizaji wa mafuta, hatua ambayo imechochea ukuaji wa uchumi na kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa nishati nchini.

Katika miaka minne iliyopita, PBPA imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa weledi na mafanikio makubwa, ikijumuisha kupunguza gharama za uagizaji wa mafuta kupitia mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja (Petroleum Bulk Procurement System - BPS). Kupitia mfumo huu, bei ya mafuta imeendelea kuwa shindani katika soko la ndani huku upatikanaji wa bidhaa za mafuta ukiimarika.

Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS)

Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja ni utaratibu unaotumiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhakikisha kuwa bidhaa za mafuta ya petroli zinapatikana nchini kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Mfumo huu unajumuisha ununuzi wa mafuta kwa pamoja kutoka kwa waagizaji wa ndani na wa kimataifa kupitia zabuni za ushindani kwa lengo la kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini kwa gharama nafuu na ubora unaokidhi viwango.

Bidhaa ambazo kwa sasa zinaagizwa kupitia BPS ni petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege. Bidhaa hizi huagizwa kupitia zabuni zinazotangazwa kila mwezi kwa wazabuni waliokidhi vigezo. Kumekuwa na ongezeko

la zabuni kutoka 107 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia 127 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la zabuni 20. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini na nchi jirani zinazotumia bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

Wastani wa gharama za uletaji wa bidhaa za Petroli (Premiums) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 uliongezeka kwa asilimia 92.2 kwa dizeli, na kuongezeka kwa asilimia 152.7 na asilimia 165.7 kwa petroli na mafuta ya ndega/taa ikilinganishwa na premium za mwaka wa fedha 2021/2022. Uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli umeongezeka kwa asilimia 12.1 kuongezeka kwa uagizaji wa mafuta kunachangiwa ukuaji wa uchumi, ikizingatiwa kuwa Pato la Taifa (GDP) lilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2023 na linatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2024 kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Uagizaji wa ndani umeongezeka kwa asilimia 10.9 na uagizaji wa mafuta ya matumizi ya nchi jirani umeongezeka kwa asilimia 13.1. Ongezeko hilo limetokana na ukuaji wa uchumi na nchi hizo na kuongeza matumizi za Tanzania kupitisha shehena za mizigo yao katika bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

## MFUMO WA SCADA

Mfumo wa udhibiti wa usimamizi na upatikanaji wa taarifa (SCADA) unaotumiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) ili kupata taarifa za papo kwa papo kutoka kwenye mita za Serikali na mita za kampuni wakati wa upakuaji wa mafuta kutoka kwenye meli na upokeaji wa mafuta kwenye maghala ya kuhifadhia.

Katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia, PBPA imekamilisha usimikaji wa mfumo wa kielektroniki SCADA na kuanza matumizi yake. Mfumo huu husaidia kudhibiti upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji kutoka kwenye meli na upokeaji wa mafuta kwenye maghala ya kuhifadhia.

Mfumo huu una uwezo wa kusoma kiasi cha mafuta yanayopita katika mita (flowmeter) za Serikali zilizopo Kurasini, Kigamboni, Tanga na Mtwara kulinganisha na kiasi cha mafuta yanayopita katika mita zilizopo kwenye maghala ya kuhifadhia mafuta. Upatikanaji wa taarifa hizi unawezesha Serikali kudhibiti upotevu wa mafuta.

Tangu mfumo wa SCADA kufungwa, mafanikio mbalimbali yameripotiwa, ikiwa ni pamoja na kiwango cha upotevu wa mafuta kupungua kutoka asilimia 0.5 hadi chini ya asilimia 0.1. Mfumo wa SCADA umeleta zama mpya za uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa kiutendaji katika mchakato wa uingizaji wa mafuta nchini Tanzania.

Serikali kupitia PBPA imepanga kuboresha uwezo wa mfumo huo kwa kuunganisha Mfumo wa kupima matenki moja kwa moja (ATG) kwa matenki yote ya kuhifadhia mafuta. Mfumo huu utaiwezesha Serikali kufuatilia nafasi wazi ya tanki (ullage) na kiwango cha mafuta kilichopo kwa wakati halisi hivyo kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli (demurrage) pamoja na kujua kwa hakika kiasi cha mafuta kilichopo kwenye maghala kwa wakati wote.

## Upatikanaji wa Mafuta

Uhakika wa upatikanaji wa mafuta umeongezeka kutokana na usimamizi madhubuti wa Uagizaji na kuhifadhi. Akiwasilisha taarifa ya mwenendo wa mafuta nchini kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Nishati na Madini, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko alisema kuwa, kuwa PBPA ambayo inasimamia uagizaji wa mafuta kwa pamoja, ina umuhimu mkubwa nchini kwani ndiyo inayopelekea nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi na yenye viwango vya ubora unaohitajika, Serikali kufahamu kiwango cha mafuta kinachoingia nchini, kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kutumia takwimu sahihi na kupanga bei elekezi ya mafuta. Serikali inaendelea kuisimamia kwa ukamilifu PBPA ili iendelee kufanya kazi kwa

ufanisi kwani tayari imekuwa ni mfano wa kuigwa kwa nchi zinazotuzunguka.

Aidha serikali kupitia maboresho ya Kanuni za mafuta ya petroli ya mwaka 2024 Regulation(kanuni) July 2024 na miongozo ya mafuta na petroli manual (Muongozo) imeboresha mazingira yaliyoongeza ushiriki wa wazabuni na makampuni ya mafuta kupitia

Usimamizi wa Sheria/Kanuni/Taratibu za mfumo wa BPS.

PBPA imeongeza uwezo wake wa kushughulikia masuala ya kisheria, kiufundi, na kisera katika sekta ya mafuta. Wakala umejikita katika kuhakikisha mafuta yanayopatikana nchini siyo tu yanapatikana kwa wakati, bali pia yanakidhi ubora unaotakiwa kwa usalama wa watumiaji na mazingira. Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, PBPA na Ofisi ya Wakili Mkuu ilifanikiwa kuibuka kidedea kwenye kesi iliyokuwa ikiendeshwa katika Baraza la Kimataifa la Biashara (International Chamber of Commerce-ICC) dhidi ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu. Uamuzi wa kuipa Tanzania ushindi katika Shauri la Usuluhishi Na. 2682/AZO baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement Agency-PBPA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Kampuni hiyo, umetolewa na ICC Machi 6, 2024.

Shauri hilo lilifunguliwa baada ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kushindwa kusambaza mafuta kwa mujibu wa mkataba uliotokana na zabuni Na. PBPA/CPP/PMC/C3-KOJI/02/2021 wa Januari 5, 2021 kwa ajili ya kuleta nchini mafuta, metriki za ujazo 36,192. Mafuta hayo yalipaswa kupokelewa nchini kuanzia Februari 27, 2021 hadi Machi 1, 2021.

Katika uamuzi wake, Baraza la ICC limetamka kuwa Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC ilivunja Mkataba na hivyo kuwaamuru kurejesha fedha kwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) dola za Marekani milioni tisa, laki saba na kumi elfu, mia sita hamsini na moja na senti arobaini na tano (USD 9,710,651.45) pamoja na riba kabla ya tuzo (pre-award interest) asilimia 7.67% kuanzia tarehe 18 Mei, 2021 hadi Novemba, 2023; kwa kuvunja Mkataba na kushindwa kuleta mafuta nchini. 2 Pamoja na Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kuamuriwa na Baraza hilo kurejesha fedha tajwa hapo juu kwa kuvunja Mkataba, pia Kampuni hiyo inatakiwa kutekeleza Kuilipa PBPA dola za Marekani milioni moja, laki moja arobaini elfu, na arobaini na nane (USD 1,140,048.00) ikiwa ni adhabu ya kuharibu mfumo wa ununuzi wa mafuta wa Pamoja, Kuilipa PBPA dola za Marekani laki nane themanini na mbili elfu (USD 882,000.00) ikiwa ni gharama za Baraza, Kuilipa PBPA shilingi milioni mia nane kumi na nane elfu, laki mbili themanini na tano na mia saba (TZS 818,285,700.00) ikiwa ni gharama za kesi na Kulipa riba baada ya tuzo (post award interest)

Kuongeza mchango wa sekta binafsi:

Ushirikiano kati ya PBPA na sekta binafsi umeimarika, jambo ambalo limeongeza ufanisi na kupanua wigo wa huduma za uagizaji na usambazaji wa mafuta. PBPA imekuwa ikikutana mara kwa mara na wadau mbalimbali, wakiwemo waagizaji, wasambazaji, na wamiliki wa vituo vya mafuta. Mikutano hiyo imesaidia kubaini changamoto zinazoikumba sekta hiyo na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzitatua kwa haraka. Ushirikiano huu wa wazi ni ishara ya utawala wa Rais Samia unaoweka mbele mazungumzo na maridhiano kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Chini ya uongozi wa Rais Samia, PBPA imeongeza ushirikiano wake na taasisi kama EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji), TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), TPA (Mamlaka ya Bandari Tanzania) na TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania). Ushirikiano huu umesaidia kurahisisha uratibu wa mchakato wa uagizaji, utoaji na usambazaji wa mafuta nchini. Kwa mfano, kwa kushirikiana na EWURA, bei za mafuta hutangazwa kila mwezi kwa uwazi, hatua inayotoa fursa kwa wananchi kujua bei halali na kuondoa usumbufu wa kupandishwa kiholela kwa bei vituoni.

Mchango wa Serikali katika kuimarisha Biashara ya Mafuta


Kwa kutumia mbinu za kisasa za usimamizi

na teknolojia, Kupitia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imeanza kuona matunda ya uwekezaji katika sekta ya nishati, hususan mafuta. PBPA, kama sehemu ya taasisi muhimu chini ya Wizara ya Nishati, imekuwa chachu ya mageuzi haya. Mwelekeo huu unadhihirisha dhamira ya serikali kuijenga Tanzania mpya yenye uchumi wa kisasa, uwazi wa kiuongozi, na huduma bora kwa wananchi

Utawala Bora na Usimamizi wa Kimkakati (Governance and Strategic Oversight)

PBPA imeendelea kusimamia na zimeboresha uandishi wa taarifa zake za hesabu na kupelea kuendelea kupataHati safi kwenye ukaguzi wa hesabu za mwaka wa Fedha katika kipindi cha miaka 4 ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu. Aidha PBPA imeendelea kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa na mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali CAG ili kuendelea kupata hati safi.

Aidha, PBPA imeendelea kutoa Mafunzo kwa watumishi kuhusu Maadili, Kudhibiti Rushwa kwa lengo la kuwajenga watumishi katika maadili mazuri na kukabiliana na vitendo vya rushwa maeneo ya kazi.




***Mchoro wa mtiririko wa mchakato wa kushusha na kuhamisha bidhaa za mafuta ya petroli***



# MFUMO WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA WAENDELEA KUIMARIKA- DKT. BITEKO

*Mhe. Dkt Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akiwasilishwaji wa bajeti ya wizara ya nishati 2025/2026 bungeni Dodoma*

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imeendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement System - BPS) katika uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini tangu ulipoanza kutumika mwezi Januari 2012.

Akiwasilisha bajeti ya Wizara ya Nishati tarehe 28 Aprili 2025 bungeni jijini Dodoma, Dkt. Biteko alieleza kuwa kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya lita bilioni 6.74 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliagizwa. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 7.3 ikilinganishwa na lita bilioni 6.28 zilizoagizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Alifafanua zaidi kwamba, kati ya kiwango hicho cha mafuta, petroli ilikuwa lita bilioni 2.23, dizeli lita bilioni 4.24, na mafuta ya taa/ndege lita milioni 270. Bidhaa hizo zilipokelewa kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Aliongeza kuwa kati ya mafuta hayo



*Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakiwa bungeni jijini Dodoma ikiwa ni siku ya uwasilishwaji wa Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2025/2026.*

yaliyoagizwa katika kipindi husika, lita bilioni 3.26 (sawa na asilimia 48) yalikuwa kwa matumizi ya ndani, ikilinganishwa na lita bilioni 3.37 mwaka 2023/24. Vilevile, lita bilioni 3.48 (sawa na asilimia 52) ziliagizwa kwa matumizi ya nchi jirani, ikilinganishwa na lita bilioni 2.9 mwaka 2023/24. Mafuta kwa ajili ya nchi jirani

yaliongezeka kwa asilimia 16 kufuatia kuimarika kwa ufanisi wa mfumo wa PBPS, hali ambayo imezifanya nchi hizo kuendelea kuvutiwa kutumia mfumo huo.

Kuhusu zabuni za mafuta, Dkt. Biteko aliongeza kuwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya zabuni 100 zilitangazwa kwa ushindani wa kimataifa kwa kuzingatia kigezo cha gharama ndogo za uagizaji wa mafuta nchini (lowest premium). Aidha, kila mwezi kulitangazwa zabuni 10 hadi 13 ambazo zilishirikisha jumla ya wazabuni 9 hadi 10, wakiwemo pia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Ushiriki wa TPDC ulichochea ushindani na kuongeza uwazi katika uagizaji wa mafuta, na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uagizaji wa mafuta nchini.

Dkt. Biteko alisema kuwa Serikali kupitia PBPA imeendelea kuongeza ufanisi wa usimamizi wa upakuaji mafuta kutoka melini hadi kwenye hifadhi za makampuni ya mafuta kwa kutumia mfumo wa udhibiti, usimamizi na upataji wa data (SCADA). Hatua hii imeimarisha udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji kutoka melini. Mfumo huo husoma kiasi cha mafuta kinachopita katika mita (flowmeter) za Serikali kwa muda halisi, na kulinganisha matokeo hayo na kiwango cha mafuta kinachopokelewa kupitia mita za makampuni ya mafuta kwenye maghala yao ya kuhifadhi.Uwepo wa mfumo huu umepunguza upotevu wa mafuta kutoka takriban asilimia 0.5 hadi asilimia 0.1.

Dkt. Biteko alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha nchi ina uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na ufanisi katika usimamizi wa upatikanaji wa bidhaa hizo wakati wote.



*Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakiwa bungeni jijini Dodoma ikiwa ni siku ya uwasilishwaji wa Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2025/2026.*




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko,akizungumza wakati akizindua Taarifa za Maendeleo ya Sekta ya Nishati kwa Mwaka 2023/24,hafla iliyofanyika leo Aprili 9,2025 jijini Dodoma.*

# USHINDANI WAONGEZEKA SEKTA YA MAFUTA - DKT. BITEKO

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, amesema hali ya upatikanaji wa mafuta nchini unaendelea kuimarika na biashara ya mafuta imeendelea kuwa ya uwazi kutokana na kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya mafuta.

Mhe. Dkt. Biteko ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Taarifa ya EWURA kuhusu Maendeleo ya Sekta ya Nishati nchini (umeme, petroli na gesi asilia) katika hafla iliyofanyika Dodoma.

Alisema kuwa kuimarika kwa upatikanaji wa mafuta nchini kumetokana na jitihada za kuhamasisha wawekezaji wa ndani kujenga vituo vya mafuta katika miji midogo na vijijini ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa bidhaa hiyo.

Dkt Biteko alisema kuwa anaridhishwa na ushirikiano anaoupata kutoka kwa kampuni za mafuta na kusema ushirikiano huo una nia ya kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa ya mafuta kwa bei nafuu na uhakika.

Dkt. Biteko pia alionya kuwa asiwepo mtu mwenye nia ya kuvuruga na kukwamisha mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwani ndio umechangia mafanikio haya ya kuimarika kwa upatikanaji wa mafuta nchini.

Awali, Mkurugenzi Mkuu

wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dkt. James Andilile amesema sekta ya mafuta imeendelea kuimarika kutokana na ushindani wakutosha kutokana na kuwepo kwa washiriki wengi kwenye zabuni za uagizaji wa mafuta.

Dkt. Andilile alisema kuwa licha ya changamoto zilizotokana na siasa za kidunia na mabadiliko ya sera za uchumi za Marekani, nchi yetu chini ya uratibu wa PBPA iliendelea kupata mafuta wakati wote.

Dkt. Andilile alisema kuwa uzinduzi wa taarifa hizo ni takwa la kisheria na tayari wameshafanya hivyo kwa upande wa Sekta ya Maji.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli umeongezeka kwa 12.1% kuongezeka kwa uagizaji wa mafuta ya petroli kumechangiwa zaidi na ukuaji wa uchumi, ikizingatiwa kuwa Pato la Taifa (GDP) lilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2023 na linatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.7 mwaka 2024.

Uagizaji wa ndani umeongezeka kwa asilimia 10.9 na uagizaji wa mafuta ya matumizi ya nchi jirani umeongezeka kwa asilimia 13.1. Ongezeko hilo limetokana na ukuaji wa uchumi katika nchi jirani na matumizi makubwa zaidi ya bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

Aidha, taarifa inasema kuwa kwa mwaka 2023/2024 PBPA ilitangaza jumla ya zabuni 116 kwa waagizaji wa bidhaa ya mafuta ambalo ni sawa na ongezeko la zabuni 9 kutoka zabuni 107 kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko la idadi ya zabuni limechangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini na nchi jirani zinazotumia bandari ya Tanzania.




*Sehemu ya washiriki wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko,(hayupo pichani) wakati akizindua Taarifa za Maendeleo ya Sekta ya Nishati kwa Mwaka 2023/24,hafla iliyofanyika leo Aprili 9,2025 jijini Dodoma.*



# WAZIRI SIMBACHAWENE AWAPONGEZA PBPA

*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, akipata maelezo ya namna Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) inavyotekeleza majukumu kutoka kwa Bi. Hilda Kowero, Afisa Logistiki wa Mafuta.*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, amepongeza Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa namna inavyotekeleza majukumu yake katika kuhakikisha upatikanaji wa mafuta wa uhakika.

Waziri Mhe.Simbachawene alitoa pongezi hizo tarehe 17 Juni,2025 alipotembelea banda la PBPA katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika viwanja vya Chinangali Park, Dodoma,

"Nawapongeza sana mnafanya kazi nzuri katika kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa mafuta umeongezeka kutokana na usimamizi madhubuti wa Uagizaji na uhifadhi wa mafuta nchini" Mhe Simbachawene

Akielezea utekeleza wa majukumu ya Wakala kwa Mhe. Simbachawene, Afisa Logistiki ya Mafuta (PBPA), Bi. Hilda Kowero alisema majukumu ya msingi ya Wakala kuwa ni pamoja na kuratibu Mfumo wa Uagizaji mafuta kwa pamoja na kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu ameipongeza PBPA kwa uratibu mzuri na kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini kwa wakati wote.

Mhe. Naibu Waziri ameyasema hayo 20 Juni, 2025 alipotembelea banda la Wakala wakati wa maonesho ya wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

Amesema kuwa chini ya Wakala uhakika wa upatikanaji wa mafuta umeongezeka kutokana

na usimamizi madhubuti na kuongezeka kwa uhakika wa usalama wa nishati ya mafuta nchi.

Mhe. Sangu amesema kuwa PBPA imefanya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aendelee kuwahudumia watanzania kwa utulivu kwa kuweza kufanya kazi vizuri ipasavyo na kutuliza suala la upatikanaji wa mafuta kwa miaka yote.

"PBPA imeweza kuweka utaratibu mzuri ambao nchi yetu hatupati tena upungufu wa mafuta, nchi yetu hatupati migogoro na mpaka majirani zetu wengine wanapata shida sisi tunakuwa bado tuna hifadhi ya kutosha" amesema Mhe. Sangu

Aidha, Mhe. Sangu amesema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ipo tayari kutoa msaada kwa jambo lolote linayohusiana na ofisi yake kwa PBPA pale ambapo utahitajika.

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeshirika Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma na kutoa elimu kwa wadau na wananchi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wakala.

Maadhimisho hayo yameanza leo Juni 16, 2025 katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma, yanaratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambapo kwa mwaka huu 2025 yanabebwa na kaulimbiu inayosema " Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti ili kuongeza Upatikanaji wa Taarifa za Kuchagiza Uwajibikaji".




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akipata maelezo ya namna Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) inavyotekeleza majukumu kutoka kwa Bi. Hilda Kowero, Afisa Logistiki wa Mafuta.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu(katikati) katika picha ya pamoja na watumishi wa PBPA alipotembelea Banda kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 jijini Dodoma.*




*Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakitoa elimu kwa umma kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala katika ya Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.*

# PBPA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA KWA MWAKA 2025

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeungana na Taasisi nyingine za Serikali katika kushiriki Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2025, yaliyoanza rasmi tarehe 16 Juni 2025 katika viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma.

Maadhimisho haya yameandaliwa na kuratibiwa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yakiwa na kaulimbiu isemayo: "Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali ili Kuongeza Upatikanaji wa Taarifa za Kuchagiza Uwajibikaji." Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa teknolojia ya kisasa katika kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Katika maadhimisho haya, PBPA imeendelea kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake, hususan namna Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja unavyofanya kazi na mchango wake katika kuhakikisha upatikanaji wa mafuta nchini. Watalaam kutoka Wakala wameelezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kupitia mfumo huu, ikiwa ni

pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wazabuni wanaoshiriki katika uagizaji wa mafuta kwa pamoja; uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa wakati wote; kuimarika kwa udhibiti wa upotevu wa mafuta na kuendelea kutekeleza ajenda ya kitaifa ya Nishati Safi ya Kupikia kwa kutoa elimu kwa umma.

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika huadhimishwa kila mwaka tarehe 23 Juni na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU). Lengo la maadhimisho haya ni kutambua na kuthamini mchango wa Watumishi wa Umma katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa mataifa yao na Bara la Afrika kwa ujumla.


Kwa kushiriki katika maadhimisho haya, PBPA inaendelea kuthibitisha dhamira yake ya kutoa huduma bora kwa umma na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa mifumo madhubuti ya kiutawala na utoaji huduma, kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa na ushirikishwaji wa wananchi.




*Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala Wizara ya Nishati, Bw. Wilson Nyamanga, akipokea zawadi kutoka kwa Mhandisi Nyaronga wa PBPA kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.*




*Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakitoa elimu kwa umma kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala katika ya Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.*




*Mchoro wa mtiririko wa mchakato wa kushusha na kuhamisha bidhaa za mafuta ya petroli*

# PBPA YAPUNGUZA UPOTEVU WA MAFUTA KWA TEKNOLOJIA YA SCADA

Katika juhudi za kuimarisha uwazi, ufanisi na usimamizi wa rasilimali muhimu kwa uchumi wa Taifa, maboresho makubwa yanaendelea kufanyika katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Mabadiliko haya hayaletwi na ujenzi wa miundombinu mipya pekee, bali pia na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika udhibiti na upatikanaji wa data.

Kupitia mfumo wa udhibiti na upatikanaji wa data (Supervisory Control and Data Acquisition – SCADA), Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imepiga hatua kubwa katika kudhibiti upotevu wa mafuta na kuimarisha uwazi katika mnyororo wa usambazaji wa bidhaa hiyo nchini.

Kwa muda mrefu, bandari ya Dar es Salaam, ikiwa lango kuu la kimkakati kwa uingizaji wa mafuta nchini, imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upotevu wa mafuta wakati wa shughuli za upakuaji kutoka melini hadi kwenye matenki ya kuhifadhia. Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha upotevu huo kilizidi asilimia 0.5, hali iliyowavunja moyo wawekezaji na kuathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali.

Kutokana na changamoto ya upotevu wa mafuta, mwaka 2014 kampuni ya Petroleum Importation Coordinator Limited (PICL) – ambayo sasa inajulikana kama Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) – iliunda timu ya wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi zinazoshiriki katika mnyororo wa uagizaji mafuta. Lengo la timu hiyo lilikuwa kufanya tathmini ya hali halisi na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kupunguza upotevu wa mafuta.

Miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na timu ya

wataalamu yalikuwa kwamba kampuni zinazoagiza mafuta zifunge mita za kupima mtiririko (Inlet Flow Meters) kwenye kila njia inayosafirisha mafuta kuelekea kwenye maghala ya kuhifadhia. Vilevile, timu ilipendekeza kuwa PBPA, kama mratibu wa shughuli za uagizaji na upokeaji wa mafuta nchini, ifunge mfumo wa SCADA kwa ajili ya kusoma na kurekodi kiasi cha mafuta kinachopita kwenye mita wakati wote wa shughuli za upakuaji.

Lengo kuu la kusimika mfumo wa SCADA ni kudhibiti upotevu wa mafuta yanayoingizwa nchini pamoja na kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na taarifa muhimu za mafuta. Malengo mengine ya mfumo huu ni kufuatilia kwa wakati halisi (real time) shughuli za upakuaji wa bidhaa za mafuta kutoka melini na kubaini uchepushaji au uvujaji endapo utatokea.


Kupitia mfumo huu, maafisa wa PBPA wanaweza kubaini kwa haraka hitilafu au tofauti yoyote inayojitokeza na kutoa maelekezo stahiki. Mfumo huu umewezesha kupunguza upotevu wa mafuta na kuhakikisha kuwa mafuta yanafika kwenye maghala yaliyokusudiwa. Tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa SCADA, mafanikio makubwa yameripotiwa, ikiwemo kupungua kwa upotevu wa mafuta kutoka zaidi ya asilimia 0.5 hadi chini ya asilimia 0.1.

Aidha, usimamizi wa moja kwa moja umeongeza uwajibikaji miongoni mwa wadau wanaohusika katika mnyororo wa uagizaji na usambazaji wa mafuta. Mfumo umechangia kulinda mazingira kwa kupunguza uwezekano wa kumwagika kwa mafuta wakati wa upakuaji.

Pamoja na mafanikio hayo, PBPA imepanga kuboresha uwezo wa SCADA kwa kuunganisha mfumo mwingine wa kidijitali unaojulikana kama Automatic Tank Gauging (ATG). Mfumo huu utaiwezesha Serikali kufuatilia kwa wakati halisi ujazo na kiasi cha mafuta kwenye maghala ya kampuni za uagizaji mafuta, hivyo kupunguza gharama za ucheleweshaji wa upakuaji wa mafuta (demurrage).

Kwa kuwekeza kwenye teknolojia ya kidijitali ya SCADA, Sekta ya Nishati imeanza ukurasa mpya katika usimamizi wa biashara ya mafuta. Mfumo huu si tu kwamba umeleta uwazi na ufanisi, bali pia umejenga imani mpya kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla. Kwa mara ya kwanza, mafuta yanapokelewa, kuhifadhiwa, kusimamiwa na kuhamishwa kwa uwazi na kwa kuzingatia taarifa sahihi, hatua inayobadilisha kabisa taswira ya Sekta ya Nishati nchini.

**SBM DISCHARGE POINT**





*Wakili Hassan Dunia kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) akiwasilisha mada kwenye Mafunzo ya Sheria ya Ulinzi wa mtoa taarifa wa vitendo vya rushwa kwa watumishi wa Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).*

# PBPA YAFANYA MAFUNZO YA ULINZI WA MTOA TAARIFA

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imefanya mafunzo juu ya Sheria na Kanuni za ulinzi wa watoa taarifa kwa watumishi yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kumlinda mtoa taarifa na ushahidi wakati wa kutekeleza majukumu ya Serikali.

Akiwasilisha mada, Wakili Hassan Dunia kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) alisema kuwa mtu yeyote anaweza kutoa taarifa kwa maslahi ya umma mbele ya Mamlaka Husika ikiwa mtu huyo ana imani ya msingi kwamba kosa la jinai limefanyika, linakaribia kufanyika au kuna uwezekano mkubwa wa kufanyika; mtu mwingine hajazingatia sheria, yuko katika mchakato wa kuivunja au kuna uwezekano mkubwa wa kuivunja sheria ambayo inamwekea wajibu mtu huyo.

Bw. Dunia alieleza kuwa mtoa taarifa (whistleblower) anaweza kufichua kosa au ukiukwaji kwa mtu mwenye mamlaka katika eneo husika au kwa mtu ambaye mtoa taarifa ana imani naye, na mtu huyo atawasilisha taarifa hiyo kwa Mamlaka Husika.

Bw. Dunia alisema changamoto kubwa inayojitokeza kwenye Sheria hiyo ni wapokeaji taarifa kutotunza siri baada ya kupokea taarifa kitu ambacho

kimekuwa changamoto sana kwani inaleta udhaifu wa namna ya kukabiliana na wahalifu baada ya kupokea taarifa. Kwa Kanuni na Sheria hii inaruhusu utanzaji wa siri ili mtoaji wa taarifa alindwe.

Alieleza kuwa mamlaka husika itamlinda mtoa taarifa endapo kuna imani au hofu ya msingi kutoka kwa mtoa taarifa kwamba, kutokana na taarifa aliyoitoa anaweza kufukuzwa kazi, kusimamishwa kazi, kunyanyaswa, kubaguliwa, kutishwa au kufanyiwa aina nyingine yoyote ya unyanyasaji au kisasi na mwajiri wake au wafanyakazi wenzake.

Aidha, Bw. Dunia alisema kuwa pale ambapo mtoa taarifa atatoa taarifa kwa njia ya mazungumzo (mdomo) au kwa kutumia lugha ya ishara, Mamlaka Husika aliyepokea taarifa hiyo italazimika kuhakikisha taarifa hiyo inawekwa kwa maandishi ikijumuisha maelezo yote kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 5.

Mada hiyo ya kanuni inayoitwa The Whistleblower and Witness Protection Act, 2022 inaelezea namna ya kutoa ulinzi kwa watoa taarifa (Whistleblowers) na mashahidi dhidi ya vitendo vya kisasi au unyanyasaji; kuweka utaratibu wa kisheria wa kuwazawadia na kuwalipa fidia watoa taarifa na mashahidi, na masuala mengine yanayohusiana.







*Baadhi ya Watumishi wa PBPA wakimsikiliza mtoa mada kwenye mafunzo ya TAKUKURU.*

# MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF) UMETOA ELIMU KWA WATUMISHI WA OFISI YA WAKALA WA UAGIZAJI MAFUTA KWA PAMOJA (PBPA)

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umetoa elimu kwa watumishi wa Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhusu vifurushi, na huduma zinazotolewa na mfuko huo kwenye matibabu na kuanzishwa kwa mpango wa huduma za ziada.

Akiongea katika Mafunzo hayo Bi. Hellen Patrick, Afisa Wanachama (NHIF) kutoka Ilala amesema ili kuhakikisha huduma bora za matibabu zinapatikana kwa wanachama wake, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanzisha mpango wa huduma za ziada kwa waajiri wanaohitaji huduma hizo.

Amesema kuwa wanufaika wa mpango huo ni waajiri wote waliosajiliwa na NHIF ambapo Mwajiri anayo fursa ya kuchagua huduma za ziada kulingana na mahitaji yake.

Bi. Patrick amesema kuwa, kupitia mpango huo mwanachama anapewa fursa ya kuongeza huduma za ziada atakazopenda kulingana na mahitaji yake kwa makubaliano maalum kati ya mwajiri na NHIF.

Dkt Kunja Elihuruma ameongeza kuwa huduma zinazohusika na mpango huo ni Pamoja na; matibabu ya nje ya nchi, uchunguzi wa afya (medical checkup), dawa zilizo nje ya kitita cha mafao, gharama za ziada za miwani, kulazwa katika wodi binafsi (private ward), huduma za dharura na




*Dkt Kunja Elihuruma akiwasilisha mada ya huduma zinazohusika huduma zinazotolewa na mfuko huo kwenye matibabu kwa watumishi wa PBPA (hawapo pichani)*

uokoaji kwa kutumia ndege au gari la wagonjwa (Air and Ground Ambulance), na huduma za haraka za matibabu (Fast tracking services).

Amesema kuwa ili mwanachama aweze kunufaika na mpango huu, mwajiri anahitajika kuwa na sifa na vigezo vifuatavyo; awe mwajiri aliyesajiliwa na Mfuko, kuwasilisha fomu ya maombi kupitia mfumo, na kulipa malipo ya ziada kwa ajili ya huduma hizo mwanzoni mwa mkataba.

Ameongeza kuwa mfuko huo umekuwa ukihakikisha kuwa mwanachama anahudumiwa kulingana na michango inayotolewa na mwajiri kwa ajili ya matatibabu na kuwataka watumishi kuzingatia miongozo inayotolewa kuhusu matumizi ya huduma za ziada zinazogharamiwa na mwajiri na kuepuka gharama zisizo za lazima zinazotokana na mambo yasiyohusiana na matibabu.

Mafunzo hayo yamehusisha watumishi wa kada zote na pia ni mwendelezo wa mafunzo yanayotolewa na PBPA kwa watumishi wake ili kuwajengea uelewa wa pamoja kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu.

*Bi. Hellen Patrick, Afisa Wanachama (NHIF) kutoka Ilala akiwasilisha mada ya vifurushi na kuanzishwa kwa mpango wa huduma za ziada kwa watumishi wa PBPA (Hawapo pichani)*







*Baadhi ya Watumishi wa PBPA wakimsikiliza mtoa mada kwenye mafunzo ya NHIF.*

**The United Republic of Tanzania**
**Petroleum Bulk Procurement Agency**
**P. O. Box 2634,**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**info@pbpa.go.tz**
**+255 222 129 009**

PbpaTanzania PbpaTanzania pbpa_tanzania